katika Kituo cha Polisi KAHAMA na kupewa kumbukumbu namba KAH/RB/435/2020.
Yeyote atakae iyona haipeleke katika Kituo cha Polisi chochote kilicho karibu naye au awasiliane na kwa simu Na.0755484652.

658



MKUU wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge (kushoto), akimkabidhi nyaraka za ofisi Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, Dar es Salaam, juzi. (Na Mpigapicha Wetu).

kama utalii wa mbuga za wanyama, uwepo wa madini na biashara ya mazao, hivyo wafanyabiashara wangeweza kuutumia uwanja huo kwa shughuli za uchukuzi," alieleza.

Alisema ni muhimu serikali ikatoa majibu ya kutosha kuhusu hatma ya ujenzi wa uwanja huo wa ndege ambao wananchi wameusubiri wa muda mrefu bila kupata matumaini.

Waziri Mkuu Majaliwa mgeni rasmi maadhimisho ya utafiti na ubunifu

Na ATHNATH MKIRAMWENI

WAZIRI Mkuu Kassimu Majaliwa anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika maadhimisho ya sita ya Wiki ya Utafiti na Ubunifu yaliyoandaliwa na Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam (UDSM) yanayotarajiwa kuanza Mei 24 hadi 26 mwaka huu.

Akizungumzia jana Jijini Dar es Salaam, Naibu Makamu Mkuu wa UDSM anayeshughulikia utafiti, Profesa Bernadeta Killian, alisema maadhimisho hayo yanabebwa na kauli mbiu isemayo "Utafiti na Ubunifu kwa maendeleo Endelevu ya Viwanda na Jamii Tanzania."

Alisema chuo hicho kinatumia fursa hiyo kujipambanua katika utafiti ambao ni mojawapo ya majukumu yake kwa kuonyesha shughuli zake za utafiti, ubunifu, huduma kwa jamii na ubadilishaji maarifa katika kutatua changamoto mbalimbali za kijamii nchini.

Profesa Bernadeta alisema wiki hiyo itatoa fursa ya kuimarisha ushirikiano kati ya chuo hicho na wadau mbalimbali kitaifa na kimataifa.

Alisema wiki hiyo ya maadhimisho itatumika kutambua michango iliyotukuka ya wanataaluma na wanafunzi wa UDSM katika utafiti, ubunifu na ubadilishaji maarifa.

Kadhalika, alisema wakati wa kufunga maonyeho hayo Mei 26 mwaka huu, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Joyce Ndalichako, atawatuniku tuzo watafiti na wabunifu bora katika makundi 10.

Aliyataja makundi hayo ni miradi bora ya utafiti, idara zilizoingiza kiasi kikubwa cha fedha za utafiti na ubunifu, watafiti walioingiza kiasi kikubwa cha fedha za utafiti pamoja na utambuzi wa mtafiti hodari.

Naye, Mkurugenzi wa Ubunifu na Ujasiriamali, Dk. Ambrose Itika, alisema chuo hicho kinajitahidi kuwa karibu na jamii kutatua changamoto kupitia tafiti.

Maadhimisho hayo yanatarajiwa kuhudhuriwa na mfanyabiashara maarufu Mohamed Dewji ambaye atazungumzia nafasi ya sekta binafsi katika utafiti na ubunifu huku Profesa Hulda Swai, ambaye ni mtafiti kutoka Chuo Kikuu cha Nelson Mandela mkoani Arusha, atazungumzia nafasi ya vyuo vikuu katika ubunifu.

WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI
KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA MASWA
MAHALI MASWA
MAOMBI MAKUBWA NAMBA 17 YA MWAKA 2021
KATI YA
METODI LUKANDA IGONSHALYAMVA.....MWOMBAJI
DHIDI YA
1. KABOLE LYABAHAHEI
2. NDUNDA MAGUDULA
3. MALIMI MAGANIKO
4. JAMES BULUNGUTI
5. NYERERE MAKINA.....
WAJIBU MAOMBI
WITO/TAARIFA
KWA: KABOLE KABOLE LYABAHAHEI, NDUNDA MAGUDULA, MALIMI MAGANIKO, JAMES BULUNGUTI, NYERERE MAKINA POPOTE MLIPO KATIKA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.
Kwa kuwa mwombaji hapo juu amefungua maombi ya madai ya ardhi dhidi yenu katika Baraza hili la wilaya ya Maswa, maelezo ya madai yanaweza kupatikana hapa Barazani mnatakiwa kuleta hapa Baraza utetezi wenu wa maandishi (WSD) kabla ya tarehe 10.06.2021.
Pia mnajulishwa kuwa shauri hili limepangwa kusikilizwa siku ya tarehe 10.06.2021 saa 2:30 asubuhi mbele ya Mhe. J.T. Kaare Mwenyekiti, Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya Maswa.
Napia mnafahamishwa kuwa iwapo mtakaidi wito huu na kushindwa kutoa utetezi wa maandishi kwa muda uliopangwa Baraza litalazimika kusikiliza maombi haya upande mmoja na kutoa uamuzi dhidi yenu.
Na pia mnafahamishwa kuwa iwapo mtakaidi wito huu na kushindwa kutoa utetezi wa maandishi kwa muda uliopangwa, Baraza litalazimika kusikiliza maombi haya upande mmoja na kutoa uamuzi dhidi yenu.
IMETOLEWA kwa MKONO wangu na MHURI wa Baraza hili leo tarehe 5.05.2021.

J.T. KAARE MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) Maswa.

659

KUPOTEA KWA (CERTIFICATE OF INCENTIVES)

Kampuni ya EASTERN UNION (T) LTD inatangaza kupotelewa na Certificate of Incentives yenye No. 070297-02 iliyotolewa na kituo cha uwekezaji mwaka 2014 mwezi wa tatu.
Taarifa hii imetolewa katika kituo cha polisi cha Mbagala na kupewa kumb. Na DAR/MBA/RB/251435/2021.
Yeyote atakayekiona akipeleke katika kituo cha polisi kilicho karibu naye au awasiliane kwa simu na. 0654-844389.

661

Certified as a True Copy of the Original
Sign:.....Date:.....
GEOFREY CLARENCE LUYANJI
Advocate, Notary Public & Commissioner For Oaths